

KUMB: PPR/15 - 03/1

**TAARIFA KWA UMMA KUHUSU BEI KIKOMO ZA MAFUTA AINA YA PETROLI KUANZIA
JUMATANO, TAREHE 4 MACHI 2015**

Mamlaka ya Udhhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) inatangaza bei kikomo za bidhaa za mafuta ya petroli hapa nchini. Bei hizi zitaanza kutumika kuanzia **Jumatano, Tarehe 4 Machi 2015**. Pamoja na kutambua bei kikomo za bidhaa mbalimbali za petroli nchi nzima, ni muhimu kuzingatia yafuatayo:-

- (a) Bei za jumla na za rejareja kwa aina zote za mafuta, yaani, Petroli, Dizeli na Mafuta ya Taa zimeshuka ikilinganishwa na bei katika toleo lililopita la tarehe 04 Februari 2015. Katika toleo hili, bei za rejareja kwa Petroli, Dizeli na Mafuta ya Taa zimepungua kwa viwango vifuatavyo: Petroli Sh 116/lita sawa na asilimia 6.57 Dizeli Sh 145/lita sawa na asilimia 8.49 na Mafuta ya Taa Sh 134/lita sawa na asilimia 8.08. Aidha, kwa kulinganisha matoleo haya mawili, bei za jumla zimepungua kama ifuatavyo: Petroli, Sh 119.23/lita sawa na asilimia 7.16, Dizeli, Sh 147.94/lita sawa na asilimia 9.21, na Mafuta ya Taa, Sh 136.79/lita sawa na asilimia 8.80. Kuendelea kushuka kwa bei za mafuta katika soko la ndani kumetokana na kuendelea kushuka kwa bei za mafuta katika soko la Dunia.

Bei za mafuta masafi (*refined petroleum products*) katika soko la dunia, kwa Petroli, Dizeli na Mafuta ya Taa zimepungua kati ya mwezi Julai 2014 na Januari 2015 kwa Dola 536/tani, Dola 400/tani na Dola 440/tani sawa sawa na punguzo la asilimia 53, 46 na 48 sawa. Kati ya mwezi Septemba 2014 na Machi 2015 bei za Petroli, Dizeli na Mafuta ya Taa katika soko la ndani zimepungua kwa jumla ya kiasi cha Sh 615/lita, Sh 528/lita na Sh 517/lita sawa ambayo ni sawa na punguzo la asilimia 27, 25 na 25, sawa. Katika kipindi husika, thamani ya shilingi ya Tanzania kulinganisha na dola ya Marekani ilishuka kwa asilimia 8. Bei ya mafuta kwenye soko la ndani ingeweza kupungua zaidi kama thamani ya shilingi isingendelee kudhoofu. Pia ni muhimu kuzingatia kuwa, kwa wastani, bei za mafuta katika soko la dunia na gharama za uagizaji (CIF) huchangia asilimia 60 ya bei ya mafuta katika soko la ndani, hivyo kiwango cha ushukaji bei katika soko la ndani hakiwezi kuwa sambamba na asilimia ya ushukaji katika soko la dunia.

- (b) Kwa mujibu wa Sheria ya Mafuta ya mwaka 2008, bei za bidhaa za mafuta ya petroli zitaendelea kupangwa na soko. EWURA itaendelea kuhamasisha ushindani kwa kutoa taarifa za bei kikomo za bidhaa za mafuta. Taarifa hizi zina lengo la kuwasaidia wadau kufanya maamuzi stahiki kuhusu manunuzi ya bidhaa za mafuta.
- (c) **Kampuni za mafuta zipo huru kuuza bidhaa za mafuta ya petroli kwa bei ya ushindani ilimradi bei hizo ziko chini ya bei kikomo (price cap) kama ilivyokokotolewa na fomula iliyopitishwa na EWURA na ambayo ilichapwa kwenye Gazeti la Serikali Na. 354 la tarehe 26 Septemba 2014.**

- (d) Vituo vyote vya mafuta vinatakiwa kuchapisha bei za bidhaa za mafuta katika mabango yanayoonekana bayana na yakionyesha bei ya mafuta, punguzo, vivutio vya biashara au promosheni zinazotolewa na kituo husika. Pale ambapo inawezekana kuchagua, wateja wanashauriwa kununua bidhaa za mafuta kutoka kwenye vituo vinavyouza mafuta kwa bei ndogo zaidi ili kushamirisha ushindani. **Ni kosa kuuza mafuta bila kuweka mabango ya bei inayoonekana vizuri kwa wateja na adhabu itatolewa kwa kituo husika.**
- (e) Wanunuzi wanashauriwa kuhakikisha kuwa wanapata stakabadhi ya malipo inayoonesha jina la kituo, tarehe, aina ya mafuta yaliyonunuliwa na bei kwa lita. Stakabadhi hiyo ya malipo itatumika kama kidhibiti cha mnunuzi wa mafuta endapo kutajitokeza malalamiko ya ama kuuziwa mafuta kwa bei ya juu kuliko bei kikomo; ama endapo utakuwa umeuziwa mafuta yenye kiwango cha ubora kisichofaa.

A: BEI ZA REJAREJA

Mji	Bei Kikomo		
	Petroli (Sh/Lita)	Dizeli (Sh/lita)	Mafuta Ya Taa (Sh/Lita)
Dar es Salaam	1,652	1,563	1,523
Arusha	1,736	1,647	1,607
Arumeru (Usa West)	1,736	1,647	1,607
Karatu	1,754	1,665	1,625
Monduli	1,742	1,652	1,612
Ngorongoro (Loliondo)	1,793	1,703	1,663
Kibaha	1,657	1,567	1,527
Bagamoyo	1,663	1,574	1,534
Kisarawe	1,659	1,570	1,530
Mkuranga	1,662	1,572	1,533
Rufiji	1,680	1,590	1,550
Dodoma	1,711	1,621	1,581
Bahi	1,718	1,629	1,589
Chemba	1,737	1,648	1,608
Kondoa	1,744	1,654	1,614
Kongwa	1,708	1,618	1,579
Mpwapwa	1,712	1,622	1,583
Iringa	1,716	1,627	1,587
Kilolo	1,721	1,631	1,591
Mufindi (Mafinga)	1,726	1,637	1,597
Njombe	1,744	1,655	1,615
Ludewa	1,782	1,693	1,653

Makete	1,775	1,686	1,646
Wanging'ombe (Igwachanya)	1,742	1,653	1,613
Bukoba	1,867	1,778	1,738
Biharamulo	1,841	1,752	1,712
Karagwe (Kayanga)	1,883	1,794	1,754
Kyerwa (Ruberwa)	1,889	1,800	1,760
Muleba	1,867	1,778	1,738
Ngara	1,833	1,743	1,703
Misenyi	1,876	1,786	1,746
Geita	1,817	1,728	1,688
Bukombe	1,806	1,717	1,677
Chato	1,838	1,749	1,709
Mbogwe	1,855	1,766	1,726
Nyang'hwale	1,832	1,743	1,703
Kigoma	1,883	1,793	1,754
Uvinza (Lugufu)	1,895	1,806	1,766
Buhigwe	1,872	1,783	1,743
Kakonko	1,840	1,751	1,711
Kasulu	1,869	1,779	1,740
Kibondo	1,847	1,758	1,718
Moshi	1,726	1,636	1,596
Hai (Bomang'ombe)	1,729	1,639	1,600
Mwanga	1,719	1,629	1,589
Rombo (Mkuu)	1,747	1,657	1,617
Same	1,712	1,623	1,583
Siha (Sanya Juu)	1,732	1,643	1,603
Lindi	1,711	1,621	1,582
Kilwa Masoko	1,686	1,596	1,557
Liwale	1,732	1,642	1,602
Nachingwea	1,740	1,650	1,611
Ruangwa	1,738	1,649	1,609
Babati	1,774	1,685	1,645
Hanang (Katesh)	1,785	1,695	1,655
Kiteto (Kibaya)	1,785	1,696	1,656
Mbulu	1,787	1,697	1,658
Simanjiro (Orkasumet)	1,806	1,717	1,677
Musoma	1,830	1,741	1,701
Rorya (Ingirijuu)	1,839	1,750	1,710
Bunda	1,821	1,732	1,692
Butiama	1,827	1,738	1,698
Serengeti (Mugumu)	1,876	1,786	1,746
Tarime	1,841	1,752	1,712

Mbeya	1,759	1,669	1,630
Chunya	1,769	1,679	1,639
Ileje	1,772	1,683	1,643
Kyela	1,775	1,685	1,645
Mbarali (Rujewa)	1,743	1,654	1,614
Mbozi (Vwawa)	1,768	1,679	1,639
Momba (Chitete)	1,777	1,688	1,648
Rungwe (Tukuyu)	1,768	1,678	1,639
Morogoro	1,677	1,588	1,548
Mikumi	1,693	1,603	1,563
Kilombero (Ifakara)	1,715	1,625	1,585
Ulanga (Mahenge)	1,726	1,636	1,596
Kilosa	1,696	1,606	1,566
Gairo	1,696	1,606	1,566
Mvomero (Wami Sokoine)	1,688	1,598	1,558
Turian	1,702	1,613	1,573
Mtwara	1,724	1,635	1,595
Nanyumbu (Mangaka)	1,773	1,684	1,644
Masaki	1,750	1,660	1,621
Newala	1,756	1,667	1,627
Tandahimba	1,750	1,660	1,620
Mwanza	1,802	1,712	1,673
Kwimba	1,838	1,748	1,709
Magu	1,810	1,720	1,681
Misungwi	1,808	1,718	1,678
Sengerema	1,834	1,745	1,705
Ukerewe	1,861	1,772	1,732
Sumbawanga	1,825	1,735	1,695
Kalambo (Matai)	1,817	1,728	1,688
Nkasi (Namanyeale)	1,838	1,749	1,709
Katavi (Mpanda)	1,860	1,770	1,730
Mlele (Inyonga)	1,838	1,748	1,709
Songea	1,775	1,686	1,646
Mbinga	1,809	1,719	1,679
Namtumbo	1,805	1,715	1,675
Nyasa (Mbamba Bay)	1,811	1,722	1,682
Tunduru	1,834	1,745	1,705
Shinyanga	1,781	1,691	1,651
Kahama	1,794	1,705	1,665
Kishapu	1,809	1,720	1,680
Simiyu (Bariadi)	1,822	1,733	1,693
Busega (Nyashimo)	1,815	1,726	1,686

Itilima (Lagangabilili)	1,825	1,736	1,696
Maswa	1,814	1,724	1,684
Meatu (Mwanhuzi)	1,821	1,731	1,691
Singida	1,743	1,653	1,613
Iramba	1,755	1,665	1,625
Manyoni	1,727	1,638	1,598
Ikungi	1,738	1,649	1,609
Mkalama (Nduguti)	1,767	1,678	1,638
Tabora	1,806	1,716	1,677
Igunga	1,760	1,670	1,631
Kaliua	1,824	1,735	1,695
Ulyankulu	1,818	1,729	1,689
Nzega	1,771	1,681	1,641
Sikonge	1,818	1,728	1,688
Urambo	1,819	1,730	1,690
Tanga	1,698	1,609	1,569
Handeni	1,678	1,588	1,548
Kilindi	1,712	1,623	1,583
Korogwe	1,691	1,602	1,562
Lushoto	1,701	1,611	1,572
Mkinga (Maramba)	1,712	1,623	1,583
Muheza	1,698	1,609	1,569
Pangani	1,705	1,615	1,575

B: BEI ZA JUMLA

Bei za Jumla - DSM	Petroli (Sh/L)	Dizeli (Sh/L)	Mafuta ya Taa (Sh/L)
Bei Kikomo	1,547.19	1,457.58	1,417.80

Felix Ngamlagosi
MKURUGENZI MKUU
EWURA